# SAMPULI YA MAOMBI (mfano tu)

## Kiambatisho A
Upeo wa Mradi

**Maelekezo**
Jaza maelezo kuhusu mradi unaopendekezwa popote palipo na visanduku vya nafasi (     ) kote katika nyaraka hii. Eleza malengo na shughuli za mradi na matokeo ya mradi wako, kwa ufasaha kadri unavyoweza. Utapimwa kulingana na mawazo yako na sio kulingana na ustadi wa tahajia zako au sarufi. Tafadhali zingatia kwa karibu maelekezo yaliyotolewa.

### 1. Taarifa za Mwombaji

| | |
|---|---|
| Jina la Shirika | Southeast Asian Refugee Alliance |
| Mtu wa kuwasiliana wa Mradi | Bopha Chan |
| Anwani | 5443 S 150th St Tukwila, WA 98188 |
| Simu | 206-555-1212 |
| Barua pepe | Chan.Bopha@gmail.com |

### 2. Taarifa za Mdhamini wa Fedha – Iwapo Zinahitajika

| | |
|---|---|
| Jina la Mdhamini wa Fedha | The Environmental Stewardship Group |
| Kitambulisho cha Kodi cha Shirikisho Nambari | 123456789 |
| Mtu wa kuwasiliana wa Mdhamini wa Fedha | Amir Jordan |
| Anwani | 1496 Wall Street, Tukwila WA 98188 |
| Simu | 206-555-3434 |
| Barua pepe | Jordan.Amir@ESG.org |

### 3. Maelezo ya Jumla ya Mradi

| | |
|---|---|
| Jina la Mradi | Mradi wa Uboreshaji wa Bustani na Ujumuishaji Wakimbizi |
| Eneo la Mradi | ☐ Burien ☐ Des Moines ☐ Federal Way<br>☐ Normandy Park ☐ SeaTac ☒ Tukwila |
| Kiasi Kilichoombwa (hadi $20,000) | $17,725 |
| Katika aya fupi, eleza lengo la jumla la mradi. Tafadhali zingatia utofauti uliopo katika jamii ambayo unaitumikia na kwa nini kuna haja ya mradi huu. | |
| Lengo la mradi huu ni kuboresha bustani ya mtaa wetu na kuifanya iwe ya kuvutia zaidi kwa idadi ya wakimbizi kutoka Asia ya Kusini Mashariki ambao wanaishi karibu. Watu wengi ambao wanaishi katika jamii yetu wamekimbia vurugu na mateso ya kisiasa na ni wapya katika eneo la Tukwila. Mradi huu utaboresha bustani ya mtaa wa karibu kwa kuongeza alama katika lugha nyingi ambazo zinasema, “Unakaribishwa hapa.” Pia, tutaongeza seti ya bembea kwa watoto ili wachezee. Mwishowe, tutakuwa na sherehe ya kukaribisha, matukio ya usafishaji wa bustani ya kila wiki, na kupanda miti wakati wa msimu wa kupukutisha majani kupanda miti 20 ya asili. | |
| Katika muundo wa orodha, eleza ni shughuli gani zitafanywa au matokeo yatakuwa nini kama sehemu ya mradi. Tafadhali kumbuka shughuli zozote ambazo zitafanywa na washirika wa mradi. | |

| |
|---|
| 1. Ushirikishaji jamii - kuwafikia wakazi ili kusaidia katika kubuni alama za bustani<br>2. Kubuni na kutengeneza alama (Kampuni ya Kubuni)<br>3. Ununuzi wa seti ya bembea<br>4. Kuajiri mkandarasi wa kuweka bembea na alama (Kampuni ya Ukandarasi)<br>5. Kuwa na siku ya kukaribisha jamii<br>6. Kuwa na matukio ya usafishaji wa kujitolea ya kila wiki<br>7. Kuwa na tukio la upandaji miti ili kupanda miti 20 na vichaka |
| Tafadhali elezea ni nini kitabadilika katika mazingira au jamii kama matokeo ya utekelezaji mradi huu. |
| Mradi huu utasababisha jamii ya karibu kuhisi imekaribishwa zaidi katika bustani ya mtaa wao. Alama zitaonesha wazi kwa lugha yao ya asili kuwa wanakaribishwa. Aidha, watoto wa mtaani ambao wanaishi katika majengo ya ghorofa watakuwa na mahali pa kuja kucheza. Tutasaidia kuunda hali ya utumishi katika jamii kwa kuwa na matukio madogo za usafishaji ya kila wiki kuanzia mwezi Machi hadi Oktoba, usafishaji ambao utaondoa taka kutoka bustanini. Hatimaye, tutapanda hadi miti 20 na vichaka ili kuongeza vivuli karibu na uwanja wa michezo na kuboresha hali ya hewa katika mtaa. |

## 4. Barua za Mapendekezo

Katika barua pepe unayowasilisha, jumuisha barua mbili za mapendekezo kutoka kwa wadau wa mradi. Ni muhimu kwa Bandari kwamba mradi wako uonyeshe msaada mkubwa kwa jamii na uendane na juhudi za jiji za kuboresha mazingira. Unaweza kujumuisha barua kutoka kwa aina nyingi za wadau, kama vile: mfanyakazi wa jiji au afisa aliyechaguliwa na mtaa, shirika mbia, mwakilishi wa shirika lingine la umma, taasisi au shule ya karibu, kiongozi wa jamii, mshirika wa biashara, msimamizi wa shule na wengine.

Tafadhali kumbuka: Ikiwa mradi wako unahitaji udhamini wa kifedha, mojawapo ya barua inapaswa kuwa barua ya kuungwa mkono kutoka kwa mdhamini wako wa kifedha.

| **Maelezo** | **Barua ya 1** | **Barua ya 2** |
|---|---|---|
| Jina | Kris Kelly | Amir Jordan |
| Cheo | Msimamizi wa Utunzaji na Uendeshaji wa Bustani, Jiji la Tukwila | Meneja wa Akaunti, Kikundi cha Utumishi wa Mazingira |
| Uhusiano na Mradi | Kuruhusu uboreshaji wa bustani | Mdhamini wa Fedha |

## 5. Ratiba

Toa ratiba ya kiwango cha juu ya matukio au matokeo katika sehemu iliyotolewa. Huenda kazi ya mradi isianze hadi makubaliano na Bandari yatekelezwe kikamilifu na lazima yakamilike ndani ya mwaka mmoja.

Mfano: Agosti 2020 – Kuwa na Tukio la Jamii

| |
|---|
| Februari 2021 – Kutia saini mkataba wa ruzuku na kuwa na mkutano wa uanzishaji mradi pamoja na jamii<br>Machi 2021- Kuzungumza na wanajamii ili kutambua lugha zinazozungumzwa na kuanza kubuni alama, kununua vifaa vya usafishaji, kuanza kuwa na matukio ya usafishaji wa bustani ya kila wiki pamoja na wanajamii<br>Aprili 2021 - Kukamilisha vibali kutoka Jiji la Tukwila ili kuweka seti ya bembea<br>Mei 2021 - Ununuzi wa seti ya bembea, kampuni ya kubuni inaunda alama za kukaribisha |

Juni 2021 - Mkandarasi anaweka seti ya bembea, jamii inakagua alama za kukaribisha kabla ya kuchapishwa
Julai 2021 – Anachapisha alama, anaweka alama
Agosti 2021 – Kuwa na sherehe ya kukaribisha
Septemba- Kupanga shughuli za kupanda miti katika msimu wa kupukutisha majani
Oktoba- Kununua mimea na miti ya asili, kuwa na tukio la upandaji miti mwishoni mwa Oktoba, kukamilisha usafishaji wa mwisho wa kila wiki katika mwaka
Matukio ya usafishaji wa taka ya kila wiki yataandaliwa kati ya Machi na Oktoba

Inaendelea kwenye ukurasa ufuatao.

# Kiambatisho B

## Bajeti na Ahadi za Rasilimali

**Bajeti ya Mradi**

Tumia sehemu zilizotolewa ili kuelezea gharama zinazohusiana na mradi uliopendekezwa. Kwa maelezo ya kina iwezekanavyo, eleza shughuli na gharama zote za vifaa.

| **Shughuli, Vifaa au Gharama zingine** | |
|---|---|
| Seti ya bembea | $5,000 |
| Mkandarasi kuweka seti ya bembea na Alama za Kukaribisha | $3,000 |
| Kubuni Alama za Kukaribisha | $500 |
| Kuchapisha Alama za Kukaribisha | $500 |
| Miti ya asili | $ 2,000 |
| Zana za kupanda miti | $ 250 |
| Mifuko ya taka, glavu na vifaa vya kuzolea taka kwa usafishaji | $100 |
| Malipo kwa mratibu wa mradi | $4,000 |
| **Ada za Idhini** (Ikiwa Zinahitajika) | |
| Kibali cha uboreshaji wa uwanja wa michezo | $400 |
| **Ada za Wadhamini wa Fedha** (Ikiwa Zinahitajika) | |
| 10% ya ada ya Mdhamini wa Fedha | $1,575 |
| **Jumla ya Bajeti ya Mradi** | $ 17,725 |

**Ahadi za Rasilimali**

Mradi wako unaweza kujumuisha mchanganyiko wowote wa chaguzi zifuatazo za ahadi za rasilimali. Tafadhali angalia Kiambatisho E kwa mifano. Tumia sehemu zilizotolewa ili uorodheshe jinsi mradi wako utakavyokidhi mahitaji ya ahadi za rasilimali ya 3:1.

| **Chaguo la Ahadi za Rasilimali** | | **Thamani** | **Ahadi za Rasilimali** |
|---|---|---|---|
| 1 | Saa za kujitolea [1]. | Saa 576 zimeahidiwa x $33.02 | $19,019 |
| 2 | Washiriki wa matukio ya elimu ya umma au shughuli zinazohusiana na mradi. | saa zimeahidiwa x $33.02 | $ |
| 3 | Saa za shughuli halisi – zilizofanywa na mradi kwa hadhira lengwa zikionyesha ushirikishaji wa kina. | saa zimeahidiwa x $33.02 | $ |
| 4 | Hesabu ya manufaa ya miti (tumia kikokotoo hiki kukadiria thamani ya miti) [2]. | Upandaji miti 20 x thamani ya mti | $36,600 |
| 5 | Kupunguza gesijoto na gharama kwa jamii za hewa ya ukaa ($50 kwa kila tani ya hewa ya ukaa iliyopunguzwa)[3]. | tani zilizopunguzwa za hewa ya ukaa x $50 | $ |
| 6 | Vifaa au huduma ambazo sio fedha zilizochangwa kutoka kwa mashirika au watu ambao hawahusiani na au hawanufaiki na mradi. | $ 550 kwa kipindi cha mwaka mmoja | $ 550 |

[1] Thamani ya saa za kujitolea katika Jimbo la Washington kwa mwaka wa 2019 ni $33.02. Jifunze zaidi hapa.

[2] Kikokotoo cha Kitaifa cha Manufaa ya Miti hutumia data kutoka Kituo cha Huduma za Misitu cha Utafiti wa Misitu iliyopo Mijini. Jifunze zaidi hapa.

[3] Gharama kwa jamii ya hewa ya ukaa inakadiriwa kuwa $50 kwa kila tani ya $CO_2$ (kulingana na thamani ya leo ya dola). Jifunze zaidi hapa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Michango ya wabia wa mradi ambayo inanufaisha mradi moja kwa moja. | $ kwa kipindi cha mwaka mmoja | $ |
| 8 | Michango ya fedha taslimu au ruzuku nyingine zilizopatikana ili kusaidia mradi. | $ fedha zilizoahidiwa zilizokusanywa | $ |
| | | **Jumla ya Ahadi za Rasilimali** | **$56,169** |

**Tamko**

Ninathibitisha hapa kuwa maelezo yaliyotolewa katika ombi hili kwa Bandari ya Seattle ni ya kweli na sahihi kwa kadri ya ufahamu wangu. (Inapaswa kutiwa saini na shirika linalowasilisha au mdhamini wa fedha, ikiwa inahusika.)

| | |
|---|---|
| Jina Lililochapishwa | Bopha Chan |
| Saini | Bopha Chan |
| Cheo | Anayejitolea, Southeast Asian Refugee Alliance |
| Tarehe | 12/1/20 |

**Orodha Hakikishi ya Maombi**

Kagua Sehemu ya III. Ratiba ya maombi ya maelezo ya tarehe ya mwisho.

1. Maombi na viambatisho lazima viwasilishwe kupitia barua pepe kwa e-submittals-sa@portseattle.org.
2. Ni jukumu la mwombaji kuhakikisha uwasilishaji wa maombi kwa wakati.
3. Mafaili lazima yawe katika muundo wa PDF unaoweza kutafutwa. PDF nyingi zinakubalika.
4. Bandari haiwezi kukubali mafaili yaliyominywa ukubwa ikiwa ni pamoja na mafaili ya .ZIP au mafaili yaliyounganishwa.
5. Ikiwa faili ni kubwa kuliko MB 10, andiko la mradi lazima liwasilishwe kwa barua pepe kadhaa na kuwekwa alama "Barua pepe 1 kati ya 5," "Barua pepe 2 kati ya 5," n.k.
6. Mstari wa kichwa cha maombi wa barua pepe unapaswa kujumuisha mradi wa Mazingira wa SKCF na jina la shirika.

Tafadhali tiki sanduku zifuatazo ili uthibitishe kuwa umekamilisha na umejumuisha nyaraka zifuatazo kwenye barua pepe yako.

☒ Kiambatisho A, Upeo wa Kazi wa Mradi

☒ Kiambatisho B, Bajeti na Ahadi za Rasilimali

    ☒ikiwa ni pamoja na Tamko lililotiwa Saini (ukurasa huu)

☒Barua Mbili (2) za Mapendekezo

    ☒Barua ya Mdhamini wa Fedha – Ikiwa Inahitajika